TANGAZO LA SERIKALI NA. 552 la tarehe 5/7/2024

SHERIA YA BENKI KUU YA TANZANIA,

(SURA YA 197)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 70(1))*

KANUNI ZA UDHIBITI WA MAZINGIRA YA MAJARIBIO YA TEKNOLOJIA YA FEDHA ZA MWAKA 2024

*Kanuni* *Jina*

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

1. Jina.
2. Matumizi.
3. Tafsiri.

SEHEMU YA PILI
SIFA NA UTARATIBU WA MAOMBI

4. Sifa.
5. Utaratibu wa maombi.
6. Masharti ya suluhisho la fedha.
7. Tathmini ya maombi.
8. Kurudia kuomba.

SEHEMU YA TATU
MAJARIBIO NA MASUALA MENGINE YAHUSIKANAYO

9. Kuanza kwa majaribio.
10. Kipindi cha majaribio.
11. Mazingira ya majaribio.
12. Taarifa ya maendeleo.
13. Kuondolewa idhini.
14. Athari za kuondolewa idhini.
15. Taarifa ya mwisho.
16. Kukamilika kwa majaribio.

SEHEMU YA NNE

MASHARTI YA JUMLA

17. Uwazi.
18. Ulinzi wa taarifa.
19. Hakimiliki.
20. Malalamiko ya Wateja.
21. Ufuatiliaji.
22. Mamlaka ya jumla ya Benki.
23. Adhabu za kiutawala.

________

JEDWALI

________

SHERIA YA BENKI KUU YA TANZANIA,

(SURA YA 197)

**KANUNI**

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 70(1))*

KANUNI ZA UDHIBITI WA MAZINGIRA YA MAJARIBIO YA TEKNOLOJIA YA FEDHA ZA MWAKA 2024

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Udhibiti wa Mazingira ya Majaribio ya Teknolojia ya Fedha za mwaka 2024.

Matumizi

2.-(1) Kanuni hizi zitatumika kwa-

(a) mtoa huduma za fedha aliyesajiliwa na Benki;
(b) kampuni ya teknolojia ya fedha inayoshirikiana na mtoa huduma za fedha aliyepewa leseni na Benki; na
(c) kampuni ya teknolojia ya fedha inayokusudia kutoa suluhisho la bidhaa za fedha na huduma zinazosimamiwa na Benki.

(2) Shughuli zitakazoendeshwa na watu walioorodheshwachini ya kanuni ndogo ya (1), zitakuwa ni zile ambazo haziangukii chini ya mfumo wa sheria uliyopo..

Tafsiri

3. Katika Kanuni hizi, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

Sura ya 197

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania;

"mwombaji" maana yake ni kampuni inayokusudia kufanya majaribio ya teknolojia ya huduma za fedha ndani ya mazingira ya majaribio ya teknolojia ya fedha yaliyodhibitiwa;

"Benki" itakuwa na maana kama iliyotolewa kwake chini ya

Sheria;

"mteja" maana yake ni mtu anayetumia bidhaa yoyote yafedha huduma zinazotolewa na Mshiriki;

"mtoa huduma za fedha" maana yake ni taasisi iliyona leseni ya kutoa huduma za fedha, inayodhibitiwa na kusimamiwa na Benki;

"suluhisho la fedha" maana yake ni bidhaa yoyote, huduma, njia ya uwasilishaji, teknolojia au muundo wa biashara na inajumuisha, malipo ya kidijitali, mikopo ya kidijitali, uhamisho wa fedha na huduma za utumaji fedha, kumjua mteja wako kidijitali, jukwaa la kidijitali, huduma za utambuzi kidijitali, huduma za usalama wa mtandao na bidhaa, uendelevu wa sekta ya fedha, huduma za fedha kwa njia ya simu, uchambuzi na matumizi ya taarifa tofauti, matumizi ya teknolojia ya daftari la hesabu iliyosambazwa, akili bandia na matumizi ya mashine ya kujifunza na aina nyingine ya bidhaa, huduma, njia ya uwasilishaji, teknolojia au muundo wa biashara kama itakavyoidhinishwa na Benki;

"teknolojia ya huduma ya fedha" maana yake ni uvumbuzi wa kiteknolojia utakaotumika katika utoaji wa bidhaa za fedha na huduma;

"kampuni ya teknolojia ya fedha" maana yake ni taasisi iliyosajiliwa ndani ya Jamhuri ya Muungano kwa ajili ya utoaji wa suluhisho la fedha iliyobuniwa katika soko;

"Mazingira ya Majaribio ya Teknolojia ya Fedha Yaliyodhibitiwa" maana yake ni utaratibu rasmi uliowekwa na Benki, ambao ndani yake, chini ya mazingira yaliyodhibitiwa, kampuni inafanya majaribio ya bidhaa mpya za uvumbuzi, huduma, njia za uwasilishaji au muundo wa biashara katika mazingira yaliyothibitiwa ; na

"soko" maana yake ni mazingira ambayo ndani yake suluhisho la fedha linatolewa kwa ajili ya matumizi;

"Waziri" itakuwa na maana sawa na maana iliyotolewa kwake chini ya Sheria;

"mshiriki" maana yake ni taasisi iliyoidhinishwa kushiriki katika Mazingira ya Majaribio ya Teknolojia ya Huduma za Fedha Yaliyodhibitiwa;

"mazingira ya kufanya majaribio" maana yake ni mazingira ya soko halisi ya ambapo mshiriki anaonesha matumizi ya teknolojia ya huduma ya fedha.

## SEHEMU YA PILI
## SIFA NA UTARATIBU WA MAOMBI

Sifa

4. Watu waliyotajwa katika kanuni ya 2(1) watakuwa na sifa za kuomba kushiriki katika Mazingira ya Majaribio ya Teknolojia ya Fedha Yaliyodhibitiwa .

Utaratibu wa maombi

5.-(1) Dirisha la maombi ya kushiriki katika Mmazingira ya Majaribio ya Teknolojia ya Fedha Yaliyodhibitiwa litafunguliwa kwa robo mwaka ambapo Benki itawakaribisha waombaji kupitia tovuti yake rasmi na vyombo vingine vya habari vilivyosambaa katika eneo kubwa.

(2) Kwa kuzingatia kanuni ya 4, mtu anayekusudia kuomba kushiriki katika Mazingira ya Majaribio ya Teknolojia ya Fedha Yaliyodhibitiwa atatakiwa kujaza fomu ya maombi kama ilivyoainishwa katika sehemu A ya Jedwali la Kanuni hizi.

(3) Fomu ya maombi iliyorejewa katika kanuni ndogo ya (2) itaambatana na-

(a) barua ya maombi kama ilivyoainishwa katika sehemu B ya Jedwali ya Kanuni hizi;
(b) nakala zilizothibitishwa ya katiba za kampuni;
(c) nakala iliyothibitishwa ya cheti cha usajili;
(d) barua halisi kutoka kwa Msajili wa Kampuni inayobainisha taarifa za kampuni;
(e) ushahidi wa vyanzo vya fedha kwa ajili ya kuwezesha majaribio;
(f) wasifu wa watendaji wakuu wa mwombaji ulioambatishwa na picha moja ya pasipoti ya hivi karibuni, nakala zilizothibitishwa za kitambulisho cha taifa au hati ya kusafiria;
(g) mkataba uliosainiwa kati ya kampuni ya teknolojia ya fedha na mmiliki wa mazingira ya majaribio endapo mwombaji ni aliyerejewa katika kanuni ya 2(1)(b) na (c);
(h) muundo wa mfumo;

(i) sera ya udhibiti wa utakatishaji fedha haramu na udhibiti wa ufadhili wa ugaidi;
(j) sera ya kumlinda mlaji wa huduma za fedha;
(k) uamuzi wa Bodi ya Wakurugenzi wa kampuni kuridhia ushiriki wa kampuni katika Mazingira ya Majaribio ya Teknolojia ya fedha Yaliyodhibitiwa;
(l) mpango halisi wa kibiashara unaoonesha jinsi suluhisho la fedha litakavyotumika baada ya kutoka katika Mazingira ya Majaribio ya Teknolojia ya Fedha Yaliyodhibitiwa;
(m) andiko la suluhisho la fedha linalojumuisha-
  (i) maelezo ya suluhisho la fedha na changamoto linalotatua;
  (ii) maelezo ya rasilimali fedha na watu zinazohitajika kwa ajili ya majaribio;
  (iii) manufaa kwa wateja;
  (iv) muda na mpango wa utekelezaji wa suluhisho la fedha unaopendekezwa;
  (v) maelezo ya mazingira ya majaribio yaliyopendekezwa na jinsi majaribio yatakavyofanyika;
  (vi) matokeo muhimu yaliyokusudiwa kutoka kwenye majaribio; na
  (vii) mkakati wa majaribio unaopendekezwa pamoja na namna ya kutoka kwenye mazingira ya majaribio ya teknolojia ya fedha yaliyodhibitiwa;
(n) taratibu zilizoandikwa zinazopendekezwa kwa ajili ya kudhibiti vihatarishi vinavyohusiana na-
  (i) amana;
  (ii) usalama mtandaoni;
  (iii) uhimilivu wa kifedha;
  (iv) ukuaji na unyumbulishwaji na uendelevu wa biashara wa suluhisho la fedha linalopendekezwa; na
  (v) kusomana kwa mifumo.

Maharti ya suluhisho la fedha

6. Suluhisho la fedha linalopendekezwa na mwombaji litatakiwa -
(a) matumizi ya teknolojia mpya au inayoibuka au matumiziya teknolojia iliyopo kwa njia ya ubunifu;

(b) kuondoa mapungufu yaliyopo katika soko au kufungua fursa mpya; na

(c) kuboresha upatikanaji, matumizi, ufanisi, usalama na ubora wa huduma za fedha.

Tathmini ya Maombi

7.-(1) Benki baada ya kupokea maombi katika kanuni 5 itafanya tathmini na kumtaarifu mwombaji kwa maandishi ndani ya siku arobaini na tano kuhusu matokeo ya tathmini na iwapo yameridhiwa au au kukataliwa kushiriki katika Mazingira ya Majaribio ya Teknolojia ya Fedha Yaliyodhibitiwa.

(2) Endapo ambapo maombi yamekataliwa na Benki, itampatia, mwombaji sababu za kwa maandishi, za kukataliwa huko.

Isipokuwa kwamba, iwapo dosari imebainikayobainika inayoweza kusababisha kukataliwa, mwombaji atapatiwa nafasi ya kuirekebisha ndani ya kipindi kilichoainishwa katika notisi ya kukataliwa.

(3) Idhini iliyotolewa chini ya kanuni ndogo ya (1) itahusika tu kumruhusu mwombaji kuendelea na majaribio ya suluhisho la fedha katika mazingira ya soko na haitachukuliwa kuwa ni idhini kamili ya kutoa suluhisho la fedha kwa umma.

Kurudia kuomba

8.-(1) Mwombaji ambaye maombi yake yamekataliwa anaweza kurudia kufanya maombi ndani ya kipindi cha miezi sita iwapo dosari iliyosababisha msingi wa kukataliwa kwa maombi ya awali imerekebishwa.

(2) Benki itatathmini maombi yaliyorudiwa na inaweza ama kuyaidhinisha au kuyakataa.

(3) Kwa madhumuni ya kanuni hii, masharti ya kanuni ya 5(1) na (2) hayatatumika katika mchakato wa maombi yaliyorudiwa isipokuwa iwapo msingi wa kukataliwa ulitokana na kutokutekelezwa kwa masharti ya kanuni hiyo.

## SEHEMU YA TATU
## MAJARIBIO NA MASUALA MENGINE YAHUSIKANAYO

Kuanza majaribio

9.-(1) Mshiriki ataanza majaribio ndani ya miezi miwili

kutokea tarehe ya kupokelewa kwa idhini kutoka katika Benki.

(2) Endapondani ya muda uliotajwa chini ya kanuni ndogo ya (1), mshiriki anashindwa kuanza majaribio atatkiwa kuwasilisha kwa Benki sababu za maandishi za kushindwa kutekeleza kwa ajili ya kuzingatiwa.

(3) Wakati wa majaribio, mshiriki -

(a) atakusanya taarifa juu ya jaribio linalofanywa;
(b) atatekeleza masharti yaliyotolewa kwenye idhini;
(c) atakeleza sheria husika;
(d) atawasilisha ripoti za maendeleo zilizoainishwa katika Kanuni hizi;
(e) atapata na kutunza idhini ya awali ya mlaji ya kushiriki katika jaribio;
(f) atazingatia vigezo na masharti ya mteja yaliyoidhinishwa kwa ajili ya majaribio ya suluhisho la fedha;
(g) atahakikisha wateja wanalindwa hususani iwapo kutokutekelezeka kunatokea;
(h) atashughulikia malalamiko ya walaji wa huduma za fedha na kulinda taarifa binafsi na za fedha;
(i) ataomba idhini kutoka Benki iwapo kuna mabadiliko katika vigezo au masharti; na
(j) atajibu maswali yote kutoka kwa Benki.

Kipindi cha majaribio

10.-(1) Mshiriki atakamilisha majaribio ya suluhisho la fedha katika Mazingira ya Majaribio ya Teknolojia ya Fedha Yaliyodhibitiwa ndani ya kipindi cha miezi kumi na mbili kutokea ya kupokelewa kwa idhini.

(2) Benki inaweza kuongeza muda wa majaribio kadri itakavyohitajika ili kushughulikia masuala mahususi au vihatarishi vilivyobainika wakati wa kipindi cha majaribio.

Mazingira ya majaribio

11. Mshiriki atafanya majaribio ya suluhisho la fedha linalopendekezwa katika mazingira ya majaribio yanayoendana na masharti yaliyobainishwa katika idhini isipokuwa kwamba, Benki inaweza kutoa masharti mengine kadiri itakavyoona inafaa.

Taarifa za maendeleo ya majaribio

12. Wakati wa majaribio, mshiriki atawasilisha kwa Benki taarifa ya maendeleo ya majaribio kila baada ya miezi

mitatu, isipokuwa kwamba, taarifa hiyo itajumuisha-

(a) mafanikio makuu yaliyofikiwa wakati wa kipindi kinachotolewa taarifa;
(b) vihatarishi vilivyobainishwa wakati wa majaribio ikijumuisha hatua za kudhibiti vihatarishi hivyo;
(c) namna ambavyo malalamiko ya wateja yalishughulikiwa;
(d) changamoto za uendeshaji zilizojitokeza na hatua zilizochukuliwa wakati wa kipindi cha majaribio;
(e) ulinzi wa taarifa binafsi na za fedha;
(f) taarifa za mabadiliko ya umiliki wa kampuni;
(g) orodha ya wateja wanaoshirikikatika Mazingira ya Majaribio ya Teknolojia ya Fedha Yaliyodhibitiwa; na
(h) taarifa nyingine yoyote ya muhimu.

Kuondolewa kwa idhini

13.-(1) Benki inaweza kuondoa idhini ya kushiriki katika Mazingira ya Majaribio ya Teknolojia ya Fedha Iliyodhibitiwa wakati wowote kabla ya kuisha kwa kipindi cha majaribio iwapo mshiriki-

(a) atashindwa kukidhi masharti ya idhini;
(b) aliwasilisha taarifa za uongo, zinazopotosha, alificha au kushindwa kuweka wazi maelezo muhimu katika maombi;
(c) anakiuka sheria yoyote inayotumika ndani ya Jamhuri ya Muungano;
(d) anafilisika;
(e) anaendesha biashara katika namna iliyona athari kwa wateja; au
(f) anashindwa kushughulikia ipasavyo kasoro zozote za kiufundi, dosari au udhaifu katika suluhisho la fedha.

(2) Benki itamtaka mshiriki kuonesha sababu ya msingi ndani ya siku kumi na nne kwanini idhini isiondolewe.

(3) Benki inaweza, iwapo itaona kuwa uwepo wa idhini utaatiri maslahi ya wateja, iwapo masharti ya kanuni ndogo ya (2) yatapaswa kutekelezwa, kuondoa idhini hiyo mara moja.

(4) Benki itawaarifu wateja kuhusu kuondolewa kwa idhini ya mshiriki katika mazingira ya majaribio kupitia vyombo vya habari vilivyosambaa katika eneo kubwa.

(5) Mshiriki anaweza, kwa ridhaa ya Benki, kujitoa kushiriki katikaMazingira ya Majaribio ya Teknolojia ya Fedha iliyodhibitiwa muda wowote kwa kutoa notisi iiyona sababu za kujitoa.

(6) Kujitoa kwa mshiriki kunaweza kuidhinishwa iwapo Benki imeridhika kuwa hakuna kosa au viashiria vyovyote kinyume na sheria au muamala uliotendwa na mshiriki katika kipindi cha majaribio.

Athari za kuondolewa kwa idhini

14.- Baada ya kuondolewa kwa idhini, mshiriki atatakiwa mara moja-

(a) atasitisha utoaji wa suluhisho la fedha kwa wateja waliopo;
(b) atawajulisha wateja kuhusu usitishwaji kwa suluhisho la fedha, haki zao za fidia itakapohitajika na wajibu wao kulipa madeni ambayo hayajalipwa; na
(c) atamfidia kwa mteja yeyote ambaye amepata hasara ya kifedha kutokana na majaribio hayo.

Taarifa ya mwisho

15.-(1) Mshiriki atatakiwa, baada ya kukamilika kwa majaribio, kuwasilisha taarifa ya mwisho inayoonesha-

(a) matokeo ya majaribio;
(b) vihatarishi vilivyobainishwa wakati wa majaribio na hatua za kudhibiti vihatarishi hivyo; na
(c) utayari wa kupeleka sokoni suluhisho la fedha lililojaribiwa.

(2) Taarifa iliyorejewa chini ya kanuni ndogo ya (1) itawasilishwa kwa Benki ndani ya siku thelathini baada ya muda wa majaribio.

Kukamilika kwa kipindi cha majaribio

16.-(1) Baada ya kukamilika kwa kipindi cha majaribio, Benki inaweza kupendekeza suluhisho la fedha kutumika sokoni.

(2) Benki inaweza kuzuia kutumika kwa suluhisho la fedha sokoni baada ya kukamilika kwa majaribio kutokana na-

(a) jaribio lililoshindikana kutokana na vigezo vilivyokubaliwa;
(b) athari hasi yasiyokusudiwa kwa umma; au
(c) tishio linaloweza kuharibu uhimilivu wa sekta ya

fedha.

## SEHEMU YA NNE
## MASHARTI YA JUMLA

Uwazi

17. Kwa madhumuni ya kuhakikisha uwazi, mshiriki atahifadhi taarifa sahihi za suluhisho la fedha zinazojumuisha-
(a) masuala yaliyobainika;
(b) udhibiti wa vihatarishi;
(c) ushiriki wa wateja; na
(d) taarifa nyingine yoyote muhimu kadri ambavyo Benki itahitaji.

Ulinzi wa taarifa

Sura ya 44

18.- Mshiriki atahakikisha kuwa taarifa zote zilizokusanywa wakati wa majaribio na, au baada ya kukamilika kwa majaribio ya suluhisho la fedha zinafanyiwa kazi kwa mujibu wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi na kwamba-
(a) taarifa zote za siri ikijumuisha taarifa binafsi za mteja zilizokusanywa wakati wa kipindi cha majaribio zinalindwa kabla ya kutoka kwenye Mazingira ya Majaribio ya Teknolojia ya Fedha iliyodhibitiwa; na
(b) taarifa zote za siri ikijumuisha taarifa binafsi za mteja zilizokusanywa wakati wa majaribio zinaharibiwa endapo idhini imeondolewa.

Hakimiliki

19.-(1) Mwombaji atakuwa na jukumu la kusajili hakimiliki yake katika mamlaka husika kwa mujibu wa sheria zinazosimamia na hakimiliki.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kanuni ndogo ya (1), Benki haitawajibika kwa madai ya hakimiliki yaliyowasilishwa na mhusika mwingine dhidi ya mwombaji au mshiriki katika Mazingira ya Majaribio ya Teknolojia ya Fedha yaliyodhibitiwa.

Malalamiko ya wateja

20.- Malalamiko ya wateja yanayotokanayo na awamu ya majaribio yatashughulikiwa kwa mujibu wa sheria zinazomlinda mlaji.

Ufuatiliaji

21. Benki -
(a) itafuatilia utekelezaji wa washiriki katika Majaribio ya Teknolojia ya Fedha Yaliyodhibitiwa; na
(b) itafanya kaguzi za maeneo kwa madhumuni ya ufuatiliaji na uhakiki.

Mamlaka ya jumla ya Benki

22. Benki inaweza, kwa vigezo na masharti kama yatakayoainsihwa, kadri itakavyoona inafaa kumuondolea wajibu wa kutekeleza masharti ya vifungu vya Kanuni hizi.

Adhabu za kiutawala

23.-(1) Mshiriki atakayevunja masharti yoyote chini ya Kanuni hizi anatenda kosa.

(2) Benki inaweza kwa kuzingatia masharti ya kanuni ndogo ya (1), baada ya kujiridhisha kuhusiana na ukiukwaji wa Kanuni hizi uliofanywa na mshiriki, kutoa amri zifuatazo:
(a) onyo; au
(b) kumsimamisha kushiriki katika mazingira ya Majaribio ya Teknolojia ya Fedha Yaliyodhibitiwa kwa kipindi cha mwaka mmoja kutokea tareheukiukwaji huo

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 5(2) na (3))*

Sehemu A

FOMU YA MAOMBI

| Maelezo ya Mwombaji | |
|---|---|
| Taarifa | Maelezo |
| Jina la mwombaji (*kampuni*) | |
| Namba ya Usajili wa kampuni | |
| Tovuti (*kama ipo*) | |
| Jina la mtu wa mawasiliano | |
| Barua pepe | |
| Namba ya simu | |
| Sanduku la Posta | |
| Anuani ya eneo la ofisi | |

Maelezo ya Wanahisa

| N.A | Jina | Utaifa | Nambari za Simu & Barua pepe | Kazi | Asilimia ya hisa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | |
| | | | | | |

Maelezo ya Wakurugenzi

| N.A | Jina | Utaifa | Cheo | Kiwango cha elimu |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |
| | | | | |

Maelezo ya suluhisho la fedha linalopendekezwa

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Eleza asili na ukubwa wa uendeshaji wa shughuli zako | *Tafadhali ufafanuzi usizidi maneno 100 na endapo kuna taarifa za ziada zinaweza kuambatishwa kama nyongeza* |
| 2. | Eleza kwa ufupi suluhisho la fedha linalopendekezwa | *Tafadhali ufafanuzi usizidi maneno 100 na endapo kuna taarifa za ziada zinaweza kuambatishwa kama nyongeza* |
| 3. | Onesha kwa ufupi chanzo cha fedha ili kuwezesha majaribio na upelekaji wa suluhisho la fedha linalopendekezwa sokoni. | *Tafadhali ufafanuzi usizidi maneno 100 na endapo kuna taarifa za ziada zinaweza kuambatishwa kama nyongeza* |
| 4. | Eleza kwa ufupi muda wa majaribio na utumiaji wa suluhisho la fedha unaopendekezwa. | *Tafadhali ufafanuzi usizidi maneno 50 na endapo kuna taarifa za ziada zinaweza kuambatishwa kama nyongeza.* |
| 5. | Eleza kwa ufupi teknolojia za msingi na miundombinu ya suluhisho la fedha inayopendekezwa sokoni. | *Tafadhali ufafanuzi usizidi maneno 200 na endapo kuna taarifa za ziada zinaweza kuambatishwa kama nyongeza* |
| 6. | Eleza kwa ufupi mahitaji ya fedha na rasilimali watu kwa ajili ya majaribio na usambazaji wa suluhisho la fedha linalopendekezwa sokoni. | "" |
| 7. | Toa maelezo ya kina ya tatizo la kutatuliwa katika mfumo wa fedha na jinsi suluhisho la fedha linalopendekezwa litakavyotatua tatizo na kutoa manufaa kwa watumiaji na/au sekta ya fedha. | "" |
| 8. | Elezea na ambatisha mpango wa biashara ukijumuisha namna ya kutumia suluhisho la fedha kwa kiwango kikubwa baada ya kuondoka kwenye mazingira ya majaribio ya teknolojia ya fedha yaliyodhibitiwa. | "" |
| 9. | Eleza mkakati wako wa kuondoka katika mazingira ya majaribio endapo utaondolewa wakati wowote au utafaulu kuingia katika soko halisi baada ya majaribio. | "" |
| 10. | Ainisha matakwa ya kisheria au ya kiusimamizi ambayo yanakwamisha utekelezaji wa teknolojia ya huduma ya fedha inayopendekezwa na marekebisho ya kiusimamizi yanayohitajika ili kufanya majaribio. | "" |
| 11. | Eleza kwa ufupi mazingira ya majaribio yanayopendekezwa na jinsi jaribio litakavyofanyika | "" |
| 12. | Eleza matokeo muhimu yanayokusudiwa katika jaribio. | "" |
| 13. | Ainisha vihatarishi ikijumuisha udanganyifu, | "" |

| | |
|---|---|
| utakatishaji fedha, ufadhili wa ugaidi na silaha za maangamizi na kutokua thabiti kwa sekta ya fedha na hatua za kudhibiti vihatarishi hivyo. | |

Tamko la Wanahisa

| | |
|---|---|
| Mimi, niliyetia saini hapa chini, natamka kwamba: | |
| a) maelezo niliyoyaainisha humu ni ya kweli na sahihi kwa kadiri ya ufahamu na imani yangu; | |
| b) sijawahi kufilisiwa au kutiwa hatiani kwa ulaghai au kukosa uaminifu; | |
| Jina: | Jina: |
| Saini: | Saini: |
| Cheo: | Cheo: |

*Tangazo La Serikali Na. 552 (Linaendelea)*

MBELE YANGU:

Jina: …………………………………………………
Saini: ……………………………………………..
Tarehe:……………………………………………
Anuani:……………………………………………
Sifa: …………………………………………………

Sehemu "B"

Mfano wa Barua

[Anuani ya mwombaji]
[Tarehe]

Gavana,
Benki Kuu ya Tanzania,
Barabara ya Jakaya Kikwete,
SLP 2303,
40184 Dodoma Tanzania.
Barua pepe: botcommunications@bot.go.tz
: info@bot.go.tz

Ndugu […………………],

RE: [Maelezo ya kukusudia kushiriki katika Mazingira ya Majaribio chini ya Benki ya Tanzania]

[Toa maelezo mafupi ya Kampuni na huduma ya fedha inayopendekezwa.]

[Toa taarifa nyingine muhimu kama vile viambatisho na namba za mawasiliano]

Wako mtiifu,

[Saini]
[Jina
[Nafasi]
[Kampuni]

Dodoma,
21 Juni, 2024

MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU
*Waziri wa Fedha*